

## KISWAHILI

JINA.....TAREHE.....

### SEHEMU A. IMLA

1. Sikiliza kwa makini sentensi utakazosomewa na msimamizi kisha ziandike kwa usahihi.

- i. \_\_\_\_\_.
- ii. \_\_\_\_\_.
- iii. \_\_\_\_\_.
- iv. \_\_\_\_\_.
- v. \_\_\_\_\_.

### SEHEMU B. MATUMIZI YA LUGHA, MSAMIATI NA SARUFI.

2. Chagua herufi ya jibu sahihi kisha iandike katika mabano.

- i. Mtoto anakula chakula kitamu. Sentensi hii ikiwa katika hali ya mazoea itakuaje?
  - A. Mtoto hali chakula kitamu
  - B. Mtoto amekula chakula kitamu
  - C. Mtoto hula chakula kitamu
  - D. Mtoto alikula chakula kitamu.[        ]
- ii. Upi ni wingi wa neno chupa?
  - A. Vyupa
  - B. Machupa
  - C. Michupa
  - D. Chupa[        ]
- iii. Neno lipi lina maana tofauti na neno **mwisho** kati ya haya yafuatayo?
  - A. Awali
  - B. Tamati
  - C. Kaditama
  - D. Katikati[        ]
- iv. Amani **amepika** ubwabwa mbichi. Katika neno amepika ni silabi ipi inaonesha hali?
  - A. A-
  - B. -me-
  - C. -pi-
  - D. -ka-[        ]
- v. Chagua neno moja ambalo ni ukanushi wa neno **lia**.
  - A. Usilie
  - B. Cheka
  - C. Nuna
  - D. Tabasamu[        ]

### SEHEMU C. METHALI, NAHAU NA VITENDAWILI

### **3. Jibu maswali kulingana na maelekezo kwa kila kipengele.**

- i. Tegua kitendawili hiki; Mzazi ana miguu mzaliwa  
hana\_\_\_\_\_
- ii. Andika kitendawili kinachoteguliwa na pichaa ifuatayo;



- iii. Andika methali inayoendana na maelezo haya;  
"Mtu asiyekiliza ushauri anaopewa na wakubwa  
zake"\_\_\_\_\_
- iv. Kamilisha methali hii; Furaha ya mzazi \_\_\_\_\_
- v. Nini maana ya nahau, "Piga pasi? \_\_\_\_\_

### **SEHEMU D: UTUNGAJI**

#### **4. Panga sentensi zifuatazo katika mtiririko ili zilete maana sahihi.**

- i. Nilikuwa chumbani kwangu nikisoma kitabu cha hadithi[ ]
- ii. Siku hiyo kulikuwa na mvua mkubwa ilioambatana na radi[ ]
- iii. Nilimsikia baba akiniita, "Mboni ! Mboni! Zima taa ulale[ ]
- iv. Ilikuwa Jumapili wakati wa usiku [ ]
- v. Nilizima taa haraka nikalala[ ]

### **SEHEMU E: UFAHAMU**

#### **5. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali uliyopewa.**

Furaha anasoma darasa la nne katika Shule ya Msingi Mwembechai. Mwalimu wake wa somo la Hisabati anaitwa Kamongo. Mwalimu Kamongo anawapenda sana wanafunzi wake. Mara zote huwaelekeza njia rahisi ya kukokotoa hesabu za kugawanya. Jana aliiingia darasani na machungwa mawili. Kisha aliyakata katika vipande sita kwa kila moja. Kisha aliwaita wanafunzi wanne na kuwaambia wagawane vipande vile. Kisha aliwaauliza , Je, kila mmoja amepata vipande vingapi? Wanafunzi wote walichemsha bongo na kunyoosha mkono juu ili wajibu swali lile.

### **MASWALI.**

- i. Mwalimu wa Furaha aliyetajwa katika habari anaitwa nani?\_\_\_\_\_
- ii. Mwalimu wa Hisabati aliiingia darasani na machungwa mangapi?\_\_\_\_\_
- iii. Wanafunzi wangapi waliitwa kugawana vipande vya machungwa?\_\_\_\_\_
- iv. Furaha anasoma shule gani?\_\_\_\_\_
- v. Je, mwaka ujao Furaha atakuwa anasoma darasa la ngapi?\_\_\_\_\_